

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

WILAYA YA CHEMBA
E-MAIL daschemba@yahoo.com
FAX/SIMU 0262963250
Unapojibu tafadhali taja:



Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
S. L. P. 126,
CHEMBA.

Kumb. Na. AB.103/441/01/70

17 Julai, 2019

WANANCHI WOTE,
WILAYANI CHEMBA.

YAH: NAFASI ZA KUKIMBIZA MWENGE WA UHURU, 2019
NGAZI YA WILAYA NA MKOA

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Mwenge wa Uhuru, 2019 unatarajia kuingia na kukimbizwa katika Halmashauri nane za Mkoa wa Dodoma Mwezi Agosti, 2019. Hivyo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya inawatangazia Vijana wote wa Wilaya yetu kuomba nafasi za kukimbiza Mwenge wa Uhuru ngazi ya Wilaya na Mkoa.

Aidha, kwa ngazi ya Wilaya wanatakiwa Vijana wanne bila kujali jinisa zao na ngazi ya Mkoa kijana mmoja tu.

Masharti:

- Kijana awe na umri kati ya miaka 18 – 35
- Awe mtanzania wa kuzaliwa
- Awe ni mwenye akili timamu
- Awe amepitia Mafunzo ya Jeshi la Akiba (Mgambo) au Jeshi lolote la Ulinzi
- Asiwe mwenye kutumia madawa ya kulevya na wala asiwe na michoro mwilini (tatoo)
- Awe anajua kusoma na kuandika.
- Aambatishe vivuli vya vyeti vyake kulingana na Elimu yake
- Barua za maombi zipitie kwa Watendaji wao wa Vijiji husika.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24/07/2019

Zahara M. Michuzi
Katibu Tawala Wilaya
CHEMBA